

MAHAKAMA KUU YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MASJALA NDOGO YA TEMEKE

(MAHAKAMA JUMUISHI YA HUDUMA ZA MIRATHI NA NDOA)

INAYOKETI TEMEKE

MAPITIO YA MADAI NAMBA 4 YA 2021

(Imetokana na uamuzi wa Mahakama ya Wilaya Ilala katika shauri la rufaa ya mirathi Na.15/2021 mbele ya Mhe. K.C. Mshomba – HM, asilia Mirathi Na. 6/2020 Mahakama ya Mwanzo Ilala mbele ya Mhe. A.P. Barasobian – HM)

BABAKEY YUSUPH KARUA.....MWOMBAJI

VERSUS

SALMA MFAUME TOFFIKI.....MJIBU MAOMBI

HUKUMU

21/2/2022 & 23/2/2022

I.C. MUGETA, J.

Mihangaiko Juma alifariki mwaka 1978. Hadi leo hii warithi wake wanahangaikia mirathi yake ambayo haijagawanywa kwao. Kumekuwa na kesi mbalimbali za mirathi kuhusu mali zake tangu miaka ya 1990 ambazo kwa sasa sitazizungumzia kwa kina. Moja ya kesi hizo ilizaa rufaa Na. 49/2001, Mahakama Kuu, Kanda ya Dar es Salaam ambapo ilielekezwa kama ifuatavyo: -

'Both the appellant and the respondent are advised to file administration proceedings in respect of Mfaume Toffiki and Asha Ismail respectively first'.

Mihangaiko Juma hakujaliwa kupata mtoto. Mfaume Toffiki na Asha Ismail walikuwa ni ndugu warithi wa Mihangaiko waliofariki bila kurithishwa mali zake zilizohusika katika rufaa tajwa. Watoto wao kwa sasa ndio wanashindania haki ya kurithi.

Kufuatia maelekezo ya Mahakama Kuu hapo juu, Msafiri Rajabu Fikirini alifungua mirathi ya Asha Ismail Katoto kupitia mirathi No 73/2016 katika Mahakama ya mwanzo Ilala. Kwa upande mwingine, Salma Mfaume Toffiki alifungua mirathi ya Mfaume Toffiki kupitia Mirathi Na. 87/2012, Mahakama ya Mwanzo Ujiji - Kigoma. Kwa muktadha huo, maelekezo ya Mahakama Kuu katika rufaa Na. 49/2001 yalishatekelezwa.

Mnamo mwaka 2020, mirathi ya Mihangaiko ilifunguliwa tena. Hii ni mirathi Na. 6/2020, katika Mahakama ya mwanzo Ilala. Mwombaji na mjibu maombi katika shauri hili waliteuliwa kwa pamoja kuwa wasimamizi wa mirathi hiyo. Pamoja na kuteuliwa huko, mwombaji alikata rufaa mahakama ya Wilaya Ilala akilalamikia, pamoja na mambo mengine, kuteuliwa kwa mjibu maombi kuwa msimamizi wa mirathi pamoja naye. Hii

ni rufaa Na. 15/2021. Baada ya kusikiliza rufaa hiyo, Mahakama ya Wilaya iliachana na sababu za rufaa zilizowasilishwa, ikafanya uchambuzi wake na kuamua kwamba wadaawa hawajatekeleza maelekezo ya Mahakama Kuu katika rufaa Na. 49/2001. Kwa ajili hiyo Mahakama ya Wilaya ilifuta na kubatilisha mwenendo mzima wa shauri la Mirathi Na. 6/2020, Mahakama ya Mwanzo Ilala.

Ni maoni na uamuzi wangu kuwa Msomi Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Wilaya alijipotosha katika kufikia uamuzi wake. Mirathi ya watu hao ilishafunguliwa kama nilivyoelezea hapo juu.

Kutokana na mkanganyiko ulioletwa na uamuzi tajwa wa Mahakama ya Wilaya, warithi waligonga mlango wa mahakama ya mwanzo Ilala kuomba mwongozo wa nini wafanye kuhusiana na mirathi Na. 6/2020 hapo mahakamani ili waweze kugawana mali za Mihangaiko Juma. Kutokana na kukosa majibu ya hoja yao, Hakimu Mfawidhi wa Mahakama ya Mwanzo alimwandikia Hakimu Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya Ilala barua yenye Kumbukumbu namba Mirathi Na. 6/2020 ya tarehe 09/09/2021 kuomba mwongozo. Hakimu Mfawidhi wa Wilaya naye alimwandikia Naibu Msajili wa Mahakama hii barua isiyo na kumbukumbu namba wala tarehe kuomba

mwongozo. Hivi ndivyo suala hili lilivyofika katika mahakama hii na baada ya kuwasilishwa kwangu na Naibu Msajili nilitoa maelekezo yafuatayo: -

'DR


Open revision file. Put initial orders and summon the parties for hearing'

Kwa tafsiri rahisi nilielekeza jalada la mapitio lifunguliwe na wadaawa waitwe ili shauri lisikilizwe. Hivyo, nani awe mwombaji na mjibu maombi kati ya wadaawa katika shauri hili imepangwa kwa utashi wa mahakama.

Mnamo tarehe 21/2/2022 wadaawa walifika mahakamani. Baada ya kuwasikiliza walikiri kwamba maelekezo ya Mahakama Kuu ya kufungua mirathi ya Mfaume Toffiki na Asha Ismail yalishatekelezwa. Hivyo waliomba mirathi Na. 6/2020, mahakama ya mwanzo Ilala iruhusiwe kuendelea ili mirathi ya marehemu Mihangaiko iweze kugawanywa na kufungwa.

Kwa vile nimeshaeleza kuwa uamuzi wa Mahakama ya Wilaya haukuwa sahihi, nimekubali ombi lao na nimeamua kuufuta katika kumbukumbu za mahakama hiyo. Maelekezo ya hukumu hiyo ya kuwatengua mwombaji na mjibu **maombi** kuwa wasimamizi wa mirathi ya marehemu Mihangaiko nayo nimeyabatilisha. Badala yake ninaelekeza kuwa Babakey Yusuph

Karua na Salma Mfaume Toffiki waendeleo kusimamia mirathi ya marehemu Mihangaiko Juma. Mirathi Na. 6/2020, Mahakama ya mwanzo Ilala nimeirejesha. Mahakama ya mwanzo Ilala inaelekezwa kusimamia kwa ukaribu mchakato wa kusimamia mirathi hiyo ili mgawanyo wa mali ufanyike na mirathi ifungwe kwa haraka itakavyowezezana.



Mugeta
I.C. MUGETA

JAJI

23/2/2022

MAHAKAMA: - Hukumu imesomwa leo hii mbele ya mwombaji na mjibu maombi.

Isw: I.C. MUGETA

JAJI

23/2/2022